



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA  
TASAC**



IMETHIBITISHWA ISO 9001:2015

## TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Tozo zilizoandalowiwa chini ya Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Tangazo la Serikali Na. 7 la mwaka 2020)

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Shirika) lilianza chini ya *kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415*, limepewa kazi, kwa mujibu wa *kifungu cha 12(1)(d) cha Sura 415*, ya kudhibiti viwango vya tozo katika huduma za usafiri kwa njia ya maji nchini. Ili kuchochea ushindani katika soko la huduma zinazodhibitiwa kwa mujibu wa *kifungu cha 5 cha Sura 415; kanuni ya 5 ya Kanuni za Tozo, T.S Na. 7/2020*, inaeleza kwamba pale ambapo Shirika litaona kuwa soko linalodhibitiwa lina ushindani ulio madhubuti, litoe Taarifa ya kuwataka watoaji wa huduma zinazodhibitiwa katika soko husika kuwasilisha kwa Shirika viwango vya tozo vitakavyotumika kabla ya kuanza kuvitumia.

Kwa kuzingatia muktadha huu, Shirika linapenda kutoa Taarifa kuwa viwango vya tozo kwa huduma dhibitiwa zilizoorodheshwa hapa chini havitahitaji idhini ya Shirika:

- (a) usafirishaji wa abiria na mizigo kwenda bandari zilizo nje ya nchi kwa njia ya maji kwa vyombo vilivyosajiliwa nchini Tanzania;
- (b) uwakala wa forodha (*clearing and forwarding agency*);
- (c) utunzaji wa makasha matupu katika bandari kavu;
- (d) utoaji wa huduma ndogondogo bandarini na melini (*miscellaneous port services*); na
- (e) huduma ya uandaaji na uwekaji shehena ya kwenda nje katika makasha (*container freight stations*).

Kwa mujibu wa *kanuni ya 5(3) ya Kanuni za Tozo za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, Tangazo la Serikali Na. 7 la mwaka 2020*, watoaji wa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanatakiwa kuwasilisha kwa Shirika kwa ajili ya taarifa viwango vya tozo vinavyotumika au vinavyotarajia kutumika kwa madhumuni ya kuvitambua na ufuatiliaji.

Mkurugenzi Mkuu  
**Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania**